

**Ghorofa ya 7, Jengo la LAPF Pension Fund, Mkabala na Kijiji cha
Makumbusho, Kijitonyama
S.L.P. 72175, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255-022 2923513-18; Nukushi: +255-22 2923519
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>**

TAARIFA KWA UMMA JUU YA UUZAJI WA MAFUTA YA PETROLI KIHOLELA

Katika siku za karibuni kumekuwa na kushamiri kwa uuzwaji mafuta hasa ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa katika maeneo yasiyoruhusiwa (nje ya vituo vya mafuta) pasipo kuzingatia masuala ya usalama na mazingira (Health, Safety and Environment).

Wauzaji hawa wa mafuta wamekuwa wakihifadhi mafuta hayo majumbani kwa kutumia mapipa, madebe, na chupa na kuyauza mitaani hasa pembezoni mwa barabara au majumbani.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji(EWURA) inapenda kutoa tahadhari kwamba utunzaji na uuzaji wa mafuta kwa namna hii ni hatari sana kwa usalama wa watu na mali, afya za wahusika na mazingira. Aidha uuzaji huo wa kiholela wa mafuta ni kinyume cha Sheria, kanuni na taratibu za nchi. Pia, ubora wa mafuta haya hauwezi kuhakikiwa na mara nyingi mafuta haya huwa hayakidhi viwango stahiki vya ubora, hivyo wanunuaji wa mafuta hayo wanahatarisha vyombo vyao na kusababisha uharibifu na gharama kubwa za matengenezo.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 131 cha Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, mtu ye yeyote anayetaka kufanya biashara ya mafuta sharti aombe na apate leseni kutoka EWURA. Kufanya biashara ya kuuza mafuta bila leseni ya EWURA adhabu yake ni faini ya **shillingi million 20** au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

EWURA inatoa **ONYO** kali kwa wote wanaojihuisha na uuzaji huu wa mafuta kiholela kuacha mara moja. Ukaguzi umeanza kufanyika nchi nzima, kwa kuhusisha pia vyombo vya usalama ili kubaini uovu huu na hatua kuchukuliwa kwa mujibu wa Sheria. Aidha, wananchi waepuke kununua mafuta haya kwani hayakidhi viwango vya ubora na ni hatari kwa vyombo vyao vya moto na pia usalama wa watu na mazingira kwa ujumla

**Imetolewa na
Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**